**O
RODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 25 Juni, 2015**

*(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)*

**Dua**

*Mhe. Spika,(Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua*

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Azimio la kufanya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2012. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Sina hakika kama kuna maelezo ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Naomba nimkaribishe.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani muhtasari wa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu Azimio la Kupitisha Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2015. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mjumbe, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. Tunaendelea Katibu.

## MAREKEBISHO YA KANUNI

### Azimio la kufanya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2012

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kazi ambayo ilikuwa inapaswa kufanyika sasa, ni hii ambayo Katibu Mezani ameitaja kwamba Waziri angewasilisha hoja hiyo ya Marekebisho ya Kanuni. Lakini utaratibu ambao huwa tunautumia ni kwamba kwanza tunaelewana katika *briefing* ya Wajumbe wote. Sasa kazi hii tuliimaliza jana wakati wa Alasiri na *briefing* kwa Wajumbe wote haikuwahi kufanyika.

Kwa hivyo, tunakusudia mara baada ya kumaliza shughuli zetu hivi punde hapa ndani, basi Wajumbe sote tukutane pale juu, ili tupeane *briefing* ya yale maeneo ambayo yanakusudiwa kufanyiwa marekebisho, kama vile ambavyo Waheshimiwa

Wajumbe wenyewe tuliomba kwa nyakati tofauti baadhi ya maeneo yaangaliwe. Kwa hivyo, shughuli hiyo tunategemea ifanyike baadae mnamo saa 6:00.

Shughuli ambayo tuifanye sasa; Waheshimiwa Wajumbe, mnakumbuka kwamba juzi juzi nilitoa taarifa ya Rais, kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anakusudia kuja kesho tarehe 26/06/2015, mnamo saa 9:30 za laasiri. Kama tunavyoelewa uhai wa Baraza hili unaanza kufikia tamati. Lakini kwa utaratibu ni lazima mwenzetu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tumuarifu ili aje.

Kwa hivyo, tuliifanya kazi hiyo na baadae atatujibu kwamba basi mimi nitakuja siku ya tarehe 26/06/2015, mnamo saa 9:30 za laasiri. Saa hizo ni humu ndani anakuja kufanya kazi yake ya kulihutubia Baraza hili na hatimaye kutoa tamko la kulivunja Baraza hili, kwa tarehe ambayo tuliitaja hapo kabla ambayo ni tarehe 13/08/2015, ndio Baraza litakuwa limevunjika rasmi. Lakini tamko hilo atalitoa Mwenyezi Mungu akitujaalia kesho.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa tunapomuita Mhe. Rais hapa tuna kawaida ya kuwaita pamoja na viongozi wengine ambao watakaa kule juu, lakini na viongozi wengine watendaji wa serikali pamoja na baadhi ya wageni tutawaalika watakaa pale juu kama kawaida. Kama vile ambavyo ilifanyika wakati wa kuanza kwa Mkutano wa Bajeti.

Kwa hivyo, Mhe. Rais kwa kawaida huwa anafuatana, na ni utaratibu ABC wake ni lazima afuatane naye, lakini bora zaidi yule ni mgeni kwa mujibu wa kanuni hawezi kuingia humu mpaka nyinyi wenyewe mkubali.

Vile vile tunamtegemea Mhe. Jaji Mkuu ambaye ni kiongozi wa Muhimili mwengine wa Mahakama naye aje, lakini yeye pia kwa mujibu wa taratibu zetu za kanuni ni mgeni. Kwa hivyo, inabidi lazima mkubali kwamba aingie humu ndani.

Pia Waheshimiwa Wajumbe, tuna Mshauri Mkuu mmoja wapo wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye ni Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na yeye pia tunategemea aingie humu ndani, na nyinyi ndio ambao mnasauti ya kuamua na kuridhia kwamba haya sawa aje, kwa sababu na yeye ni mgeni. Pamoja na nafasi hiyo lakini kwa chombo hiki hapa ni mgeni. Asiyekuwa mgeni ni Mhe. Rais tu, yeye ni mwenzetu kwa mujibu wa Katiba ni sehemu moja ya chombo hiki, Katiba Ibara ya 63 naona, yeye anapotaka kuja wakati wowote anakuja, hiki ni chombo chake ni mwenzetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kazi iliopo sasa ya kuifanya ni maombi hayo ya viongozi hao watatu, ambao nyinyi Waheshimiwa Wajumbe nitawaomba muridhie, ili kuweza kusema

kwamba haya sawa wache hawa waungane na Mhe. Rais kuingia humu ndani. Kwa hawa wageni niliowataja ni maalum, kiutaratibu na utamaduni wetu hatuwaweki pale juu, ila wanakuja huku ambako mnamuweka Spika. Angalau kwa siku ya kesho atapata wenzake wa kukaa nao huku juu, muda wote huwa mnamuacha anaongoza katika kikao hiki anakaa peke yake, lakini kwa siku ya kesho wakati wa Laasiri, basi apate na wenzake angalau wawili watatu kama mtakubali kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe, hivyo mimi naleta kwenu maombi kwamba mgeni wetu ni *ABC* wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi muridhie, ili aingie humu ndani na tumtengee nafasi yake hapa apate kuendelea na kazi yake ya kumsaidia Mhe. Rais. Naleta kwenu ombi hilo nategemea mtasema mtakavyoamua kusema. Ahsanteni, Wajumbe sijui kama mnaridhia hilo. *(Makofi)*

Makofi haya maana yake ndio mmeridhia.

**Waheshimiwa Wajumbe:** *ABC*.

**Mhe. Spika:** Eeeh! *ABC*. Kwa hivyo, ndugu yetu *ABC* wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Baraza limeridhia aingie humu ndani na tumtengee nafasi hapa juu. *(Makofi)*

Vile vile mgeni wetu mwengine maalum ni Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Omar Othman Makungu. *(Makofi)*

Makofi hayo pia yanaonesha Baraza linaridhia kwamba na yeye awe ni mmoja kati ya wageni wetu maalum na tumgengee nafasi huku juu, kwa kawaida huwa anakaa upande huu.

Mgeni mwengine maalum ni Mshauri wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ni Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad.

**Waheshimiwa Wajumbe:** Hatutaki, asije.

**Mhe. Spika:** Basi nataka nione kama huyu na yeye tunaridhia aingie maana nimesikia minong'ono kwamba hatutaki. Hebu niipate rasmi. Aje aingie humu ndani au asije?

**Waheshimiwa Wajumbe:** Asijeee!

**Mhe. Spika:** Kwa maana Baraza hili halijaridhia kwamba Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad aingie humu ndani. *(Makofi)*

Kwa kawaida masuala haya huwa hayana mjadala. Ni hoja inaletwa na Spika, inaamuliwa na mnaamua kwamba asije. Mimi ndiye ambaye nilimpelekea barua kwamba aje. Kwa hivyo, nitampelekea barua nyengine kwamba sasa kwa sababu Baraza halikuridhia kuja kwako, basi kwa heshima zote usije. Mnanipa ruhusa hiyo *(Makofi)*

Haya, hao ndio wageni wetu. Kwa kuwa tulitengeneza ratiba inayojumuisha pamoja na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ili aje humu, sasa ratiba hiyo tutairekebisha kwa mujibu wa maamuzi mliyoyafanya hivi punde. Ni sawa kabisa hiyo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivi sasa kazi ambayo tulikuwa tumeipanga tuifanye mmeshaimaliza. Kinachofuata sasa mara baada ya kusitisha shughuli zetu kwa muda, ili kwenda kupeana *briefing* hapo kwa Wajumbe wote, basi tukaifanye kazi hiyo na tutarudia kuifanya kupitisha rasmi Mwenyezi Mungu akitujaalia wakati wa saa 6:00 mchana, ili mpate kusema mawili matatu na hatimae kuipitisha hoja hii ya marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Basi Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuruni na kufikia hapa sasa nasitisha shughuli za Baraza hadi saa 6:00 mchana na kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wote tukutane hapo juu, ili kwenda kupeana *briefing,* juu ya marekebisho ya maeneo yanayokusudiwa kurekebishwa katika Kanuni zetu za Baraza. Shughuli zinasitishwa hadi saa 6:00 mchana. Ahsanteni sana.

*(Saa 9:18 asubuhi kikao kilisitishwa kwa muda hadi saa 6:00 za mchana)*

*(Saa 6.22 mchana Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Naomba sasa nimkaribishe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha tena kukutana tena katika Baraza lako hili tukufu ili kujadili mambo yetu muhimu katika shughuli za nchi yetu, na mwa mchana huu kujadili suala la Kanuni za kuendesha shughuli zetu ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, kwa kuwa hili ni jambo la Baraza la Wawakilishi na kwa kuwa Kanuni mpya inayokuja Mungu akitujaalia nitatoa nafasi maalum kwa Kamati itakayoundwa ambayo itakuwa yenyewe ndio inayowasilisha shughuli zao za Kanuni katika Baraza hili. Kwa hiyo, haitokuwa tena Waziri wa Serikali anasimama kuwasilisha Kanuni za Baraza, tunafanya hivyo kwa sasa kwa sababu ya kazi yangu ya kuliwakilisha Baraza, lakini naamini baada ya muda sio mrefu kwa kupita kwa Kanuni hizi, wenyewe Baraza la Wawakilishi watakuwa wanawasilisha Kanuni zao wakati utakapofika kufanya marekebisho yoyote ya Kanuni.

Mhe. Spika, vile vile, sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote walioshirikia katika hatua mbali mbali za marekebisho ya Kanuni zetu, miongoni mwa wajumbe hao ni wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa shughuli za Baraza, wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na wajumbe wote waliohudhuria katika kamati yetu ya *Briefing* ya Wajumbe wote wa Baraza hili, ambao kwa kiasi kikubwa walipata nafasi nzuri ya kuzungumzia kwa undani masuala yanayohusu Kanuni zetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nitoe mapendekezo na marekebisho ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar yanayotokana na mapitio yaliyofanywa ya Kanuni zinazotumika sasa, yaani Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya Toleo la 2012, lengo na mapitio haya yalikuwa kama ifuatavyo:

1. Kuangalia mahitaji ya sasa na mwenendo wa Mabunge Duniani ili iweze kuzifanya Kanuni za Baraza ziowane na mahitaji ya wakati huu na mwenendo wa Mabunge mengine duniani.

2. Kufanya uchambuzi wa desturi, mila na taratibu nzuri zinazoongoza mambo mbali mbali katika Mabunge na zinazopendekezwa sana na Jumuiya za Mabunge za Kimataifa.

3. Kutambua mabadiliko yanayotokea kwenye Mabunge ya nchi nyengine hususan kuhusu ushirikishwaji wanawake kwenye uongozi wa Mabunge, uwazi wa shughuli za Mabunge, uwajibikaji wa Serikali katika Mabunge, uwajibikaji wa Wabunge kwa wananchi na uhuru wa Mabunge.

4. Kutafakari changamoto zinazokabili Baraza la Wawakilishi na kupendekeza jinsi ya uzoefu wa Kimataifa unavyosaidia kukabiliana na changamoto zilizopo na kufanya marekebisho ya Kanuni za Baraza kwa kuzingatia mazingira ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mapitio yaliyofanywa yalielekezwa kwenye maeneo manane muhimu ambapo hata mapendekezo haya ya marekebisho ya Kanuni yamelenga sana kwenye maeneo hayo, maeneo hayo manane ni kama ifuatavyo:

1. Vyombo vya habari na uwazi katika shughuli za Kamati za Baraza.

2. Mfumo wa utaratibu wa Kamati za kudumu za Baraza na haja ya kuanzishwa kwa Kamati za Bajeti na kazi zake.

3. Njia za kuhakikishwa utekelezaji wa maazimio ya Baraza.

4. Utaratibu wa upitishwaji wa Mswada wa Bajeti, mfumo wa kudhibiti muda na utaratibu wa upigaji wa kura.

5. Uwezo na Mamlaka ya Kamati na Baraza katika upitishaji wa bajeti.

6. Nidhamu kwenye Baraza na udhibiti wa mahudhurio ya Wajumbe.

7. Ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa bajeti, muda uwa uwasilishwaji wa Rasimu ya Bajeti kwenye Baraza, nafasi ya wahusika na mazingatio ya bajeti katika kamati.

8. Mambo mengine kwa ujumla wake.

Mhe. Spika, marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kukuza demokrasia, uwajibikaji, uwazi, haki na kurahisisha kufikiwa kwa malengo ya Kikatiba ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, vyombo vya habari na uwazi katika shughuli za Kamati ya Baraza, hivi sasa Kanuni inasema kuwa shughuli za Kamati ni siri isipokuwa kama kamati itaamua vyenginevyo, inapendekezwa kwamba Kanuni ya 108 (10), irekebishwe ili itamke kwamba shughuli za kamati zitakuwa kwa uwazi isipokuwa kama kamati itaamua vyenginevyo. Sababu za marekebisho hayo ni kwamba kwanza huu ndio mtazamo unaosisitizwa katika taasisi za kibunge za kimataifa kwa mfano *CPA* na Mabunge mengine, naamini kwa kuwa Baraza letu linakwenda na wakati nalo linafuta mtazamo huo.

Mhe. Spika, marekebisho ya Kanuni ya pili kuhusu tafsiri ya neno mgeni, vile vile, marekebisho haya yanafanywa ili kuondosha wananchi wa Zanzibar kuitwa wageni

katika chombo chao hichi kitukufu ili kuwe na neno maalum litakalotumika wanapokuja wananchi wa Zanzibar, liweze kutofautishwa na wale wageni wanaotoka nje ya Zanzibar.

Mfumo wa taraibu za kamati za kudumu na haja ya kuanzishwa kwa kamati ya bajeti na kazi zake, mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni ya 9, 11 na 107(1) (a), ni kuwafanya Naibu Spika, na Wenyeviti wa Baraza wasiwe Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza isipokuwa wataendelea kuwa wajumbe wa kamati ya uongozi na shughuli za Baraza, hayo ni miongoni mwa mabadiliko yanayofanywa ili tuweka Kanuni zetu vizuri zaidi.

Mhe. Spika, marekebisho ya kuongeza Kanuni mpya 107 (9), ni kutaja wazi wazi kwenye Kanuni za kazi za Makatibu Kamati, hali kadhalika marekebisho ya kuongeza Kanuni mpya 107 (10), ni kuweka utaratibu mzuri kwa Kamati za Baraza kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

Mhe. Spika, marekebisho mengine ni pamoja na Kanuni ya 84(8), inayotoa nafasi kwa Wajumbe wenye maoni ya wachache kwenye kamati kuwasilisha wenyewe maoni yao mbele ya Baraza lako tukufu.

**Mhe. Spika, njia za kuhakikisha utekelezaji wa Maazimio ya Baraza**

Mhe. Spika, marekebisho ya Kanuni ya 108, kifungu kidogo cha 14 na 108 (15), ni kwa lengo la kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa maagizo ya Baraza zinawasilishwa baada ya miezi sita na sio baada ya mwaka mmoja kama ilivyo sasa, ripoti za mwaka za kamati zitaendelea kuwasilishwa kwenye mkutano wa Baraza wa mwezi wa March, na ripoti za utekelezaji wa maagizo ya Baraza zitawasilishwa baada ya miezi sita, yaani kwenye mkutano wa Baraza mwezi wa Septemba au Oktoba na ripoti hizo za utekelezaji zitawasilishwa kwanza kwenye kamati na baadae ndio zitaletwa barazani baada ya kufanyiwa uchambuzi na kamati na baadae ndio zitaletwa barazani baada ya kufanyiwa uchambuzi na kupata maoni ya kamati husika.

Mhe. Spika, utaratibu mwengine ni taratibu za upitishaji wa Mswada wa bajeti, mfumo wa kudhibiti muda na utaratibu wa upigaji wa kura, hivi sasa Kanuni zinatambua aina mbili za Mswada wa Sheria, aina hizo ni Mswada wa Serikali na Mswada wa Wajumbe, marekebisho ya Kanuni ya 78 yanaanzisha aina mpya ya Mswada utakaojulikana kwa Mswaada wa Kamati. Marekebisho haya yanatoa fursa kwa kamati za kudumu za Baraza kuweza kuleta Mswada wa Sheria kwenye Baraza, Mabunge ya Tanzania, Unganda na Afrika ya Kusini tayari yameanzisha na yanatumia utaratibu wa namna hiyo. Kwa hivyo, na sisi katika Kanuni zetu

tutakuwa tunapendekeza jambo hilo lifanyike baada ya Waheshimiwa Wajumbe kupitisha suala hilo.

Mhe. Spika, marekebisho mengine ni marekebisho ya Kanuni ya 92, yanapendekezwa ili kulipa Baraza fursa ya kutoa maoni kuhusu mwelekeo wa mpango wa Taifa mapema zaidi kuliko ilivyo sasa, pia, kuwezesha Kamati ya Bajeti kufikia mwelekeo huo wa mpango wa Taifa kabla haujawasilishwa kwenye baraza. Kanuni ya 94 na Kanuni ya 95, zinapendekezwa kurekebishwa ili mkutano wa bajati uanze mwezi wa Mei, badala ya Juni na pia bajeti za Wizara mbali mbali zitangulie kwanza kuwasilishwa barazani kabla ya bajeti kuu ya Serikali. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari limeanza kutumia utaratibu huo.

**Mhe. Spika, Uwezo na Mamlaka ya Kamati ya Baraza Katika Upitishaji wa Bajeti.**

Marekebisho ya Kanuni ya 98(3) yanatoa ufafanuzi kwamba kwenye Kamati ya Matumizi kila Mjumbe ataruhusiwa kutoa hoja moja tu ya kupunguza kifungu fulani ili isiwe Mjumbe mmoja huyo huyo anatoa hoja zote tatu zinazohusiana na kifungu fulani, Kanuni ya 98 (6)(b) inarekebishwa ili kufuta utaratibu wa kupunguza shilingi mia moja kutokana na kutoridhika na sera badala yake unaanzishwa utaratibu mpya wakupunguza kiasi fulani cha fedha kama ishara ya kutoridhika na jambo maalum lolote. Aidha, marekebisho ya Kanuni kwa kuongeza Kanuni mpya ya 98(8) ni kwa madhumuni ya kufafanua matokeo ya kupitisha hoja ya kupunguza shilini moja au kupunguza kiasi fulani cha fedha.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, nidhamu kwenye Baraza na udhibiti wa Mahudhurio ya Wajumbe, marekebisho ya Kanuni 58(8) yanaweka utaratibu kwamba michango ya maandishi inatolewa na Wajumbe wakati wa majadiliano kwenye Baraza iingizwe kwenye taarifa rasmi za majadiliano ya Baraza, yaani *Hansard*. Marekebisho haya ya Kanuni 66 yanafanywa ili kuongeza Kanuni mpya ya 66(2) ambayo inaanzisha Kanuni za Maadili kwa ajili yaWajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Kanuni hizo zinafanywa kwa kuwa ni nyongeza katika Kanuni za Baraza.

Mhe. Spika, halikadhalika marekebisho yanafanywa katika Kanuni 74 na Kanuni 107(6) na Kanuni mpya ya 107(7) yanakusudia kuimarisha uwajibikaji wa Wajumbe katika suala zima la mahudhurio ya Wajumbe kwenye Baraza na kwenye Kamati. Kwanza wajumbe watatakiwa kusaini orodha wa mahudhurio kwa siku, yaani asubuhi na jioni. Pili, Mjumbe asiyehudhuria kikao cha Baraza au Kamati hata kwa dharura isiyokuwa ya kufiwa na baba yake, mama, mke au mume wa mtoto hatolipwa posho za kikao ambacho hatohudhuria. Tatu, Mjumbe yeyote atakayehudhuria nusu tu ya kikao cha siku atalipwa nusu posho ya kikao kwa

mujibu alivyohudhuria. Kwa hivyo, hii inatokana na kwamba Wajumbe wa Baraza tukufu hili wanataka mahudhurio yawepo na iondokane kabisa na suala la kutokuhudhuria wakati huna sababu za msingi.

Mhe. Spika, vile vile, Kanuni imeona umuhimu wa ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa bajeti, muda wa usilishwaji wa Rasimu ya Bajeti kwenye Baraza, nafasi ya wadau na mazingatio ya bajeti katika kamati, marekebisho kwa kuongeza Kanuni 92(4) yanakusudia kuwezesha Kamati ya Bajeti kuweza kuwaalika wadau kutoa maoni yao kuhusu mwelekeo wa Mpango wa Taifa na Bajeti ya Serikali.

Mhe. Spika, mambo mengine ni marekebisho ya Kanuni ya 59(9) yanayokusudia kuimarisha utaratibu wa Mjumbe kutangaza maslahi binafsi katika jambo linaloshughulikiwa na Baraza au Kamati,  na pia inatekeleza maamrisho ya Katiba ya kumnyima haki ya kupiga kura katika jambo ambalo ana maslahi binafsi. Hii ni kwa mtu mwenye maslahi binafsi imekataza basi asitetee maslahi yake binafsi anapokuwa anafanya shughuli hizi muhimu za Baraza. Aidha, marekebisho haya yanaweka utaratibu wa Kamati ya Maadili na kinga za Wajumbe kuweza kupokea malalamiko dhidi ya Mjumbe yeyote yule atakayekiuka Kanuni hii na pia inaweka utaratibu wa Baraza kumuadhibu Mjumbe anayevunja Kanuni hii.

Mhe. Spika, marekebisho ya Kanuni ya 30 na 31 kwa ajili ya Baraza kuwa na utaratibu wenye ufanisi zaidi katika kushughulikia maombi ya wananchi na pia kuwa na utaratibu wa kutoa marejesho kwa wananchi.

Mhe. Spika, kwa kuwa baada ya maelezo hayo niliyoyaeleza mbele ya Baraza lako tukufu na kwa kuwa Kanuni hizi zinahitaji Azimio la Baraza lako tukufu, naomba kwa ruhusa yako Mhe. Spika, nisome Azimio la Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza lako ili Wajumbe wako waweze kuzipitisha na kuziunga mkono.

Mhe. Spika, kwa kuwa Kanuni za Baraza la Wawakilishi zimeweka misingi muhimu ya kuendesha shughuli za Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia utaratibu za Kibunge na kwa kufuata mila na desturi za Zanzibar na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 157 ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi. Baraza limepewa mamlaka ya kuzifanyia marekebisho Kanuni hizo za Baraza kila inapotokea na haja ya kufanya hivyo ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji bora wa shughuli za Baraza, na kwa kuwa mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni hizi yamejadiliwa na Wajumbe wa Baraza katika ngazi mbali mbali ikiwemo kamati ya uongozi na shughuli za Baraza, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya *Briefing* wa Wajumbe wote wa Baraza na merekebisho yaliyopendekeza katika vikao hivyo kuingizwa katika warka wa marekebisho ya Kanuni.

Na kwa kuwa kwa Mujibu wa Kanuni 157 ya Kanuni ya Baraza, Mamlaka ya Baraza kufanya marekebisho ya Kanuni yanapaswa kutekelezwa kwa Baraza kupitisha Azimio la kufanya marekebisho hayo, na kwa kuwa jadueli la marekebisho ya Kanuni yanayokusudiwa kupitishwa na Baraza yamewasilishwa kwa Wajumbe wa Baraza hili kuridhiwa na Wajumbe. Hivyo basi Baraza la Wawakilishi linaadhimia kuridhia na kupitishwa marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama marekebisho hayo yalivyowasilishwa kwa Wajumbe wa Baraza, kwa kadiri ya Baraza litakavyoona inafaa.

Mhe. Spika, kabla ya kutoa hoja naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana sana ndugu yetu Ibrahim Mzee *(DPP)* ambae alikuwa mtaalam wetu muelekezi katika kutengeneza Kanuni hizi, sote kama tunavyomjua ni bingwa katika eneo hili na mimi nampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. Aidha, niwashukuru sana sana ndugu zetu wa *UNDP* kwa kutoa msaada mkubwa katika kutayarisha Kanuni hizi, pamoja na kuwashukuru wote wale hususan jumuiya zote za kiraia zilizochangia katika kuboresha Kanuni hizi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kwa ruhusa yako kutoa hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa kutoa hoja ambayo imeungwa mkono, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha muhtasari wa Maoni ya Kamati naomba unigaie muda mchache kwa ruhusa yako nitoe shukurani zangu binafsi kwa kuwa hii ni mara yangu ya mwisho katika Baraza hili la nane kupata fursa ya kusimama mbele ya Baraza hili na kuwasilisha hotuba.

Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe pamoja na ofisi yako na Katibu kwa mashirikiano na malezi yako ambayo mmenipatia katika kipindi chote cha Baraza hili la nane, lakini pia shukurani za pili ziwaendee wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu kwa mashirikiano yao kwa kipindi chote tulichokuwa tukitekeleza kazi zetu, hususan Wajumbe wote waliowahi kuwa Wajumbe Kamati ya Katiba na Sheria katika vipindi vyote viwili kwa kuwa katika miaka yote mitano ya Baraza nilikuwa nikiitumikia kamati hii ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuwaomba radhi wajumbe wote ambao kwa namna moja au nyengine nimekwazana nao na nasema nimewasamehe na naombwa wale wote ambao kwa namna moja wamenikwaza mimi nimewasamehe, Mhe. Spika,

tusafiane roho zetu ili Mungu atutakabalie swaumu zetu, na *Inshaallah* tukutane tena sote katika baraza la tisa lijalo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa na kwa umuhimu wake shukurani zangu za dhati na za kipekee zimwendee mtoto wangu wa kipekee Ibrahim Mohammed Hassan kwa kunivumilia katika kipindi hichi chote ambacho mimi mama yake nikitekeleza majumu yangu, Mwenyezi Mungu amjaalie afe na siha na amkuze katika maadili mema. *Amin*.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo binafsi naomba sasa niwasilishe Muhtasari wa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Azimio la kupitisha Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi mwaka 2015.

Mhe.Spika, nachukuwa fursa hii adhimu katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia afya na uzima hata tukaweza kukutana hapa katika wasaa huu tukiwa tumefunga na huku tukifanya majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wetu katika chombo chao hiki cha Uwakilishi, *Inshaa-Allah* uwe wasaa wenye kheri, na funga zenye kukubaliwa.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha kwa kifupi sana, na kwa niaba ya Mwenyekiti, maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi yaliyowasilishwa mbele yetu punde hivi Barazani kupitia Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati naomba nimpongeze kwa kuleta marekebisho haya ya Kanuni katika wakati ambao yanahitajika sana.

Kuletwa kwa Azimio hili la mapendekezo ya kurekebisha Kanuni zetu katika kipindi hiki ni muhimu sana, kwa kuwa ni wakati muafaka sasa kufanya mapitio ya Kanuni hizo ambazo tumekuwa tukizitumia kuendesha shughuli zetu za Baraza takriban kipindi chote cha Baraza hili la Nane la Wawakilishi.

Mhe. Spika, sote tunakumbuka kuwa mara ya mwisho Kanuni hizo kufanyiwa marekebisho na Baraza hili ni katika mwezi wa Aprili mwaka 2012 ambapo Baraza hili lilikubali Azimio la Marekebisho yale kwa nia ya kuimarisha matumizi ya Kanuni hizi, na kufanya uendeshaji wa shughuli za Baraza ufanyike kwa ufanisi.

Hata hivyo ni muda mrefu umepita na mambo mengi yamejitokeza kama changamoto ambazo utatuzi wake ni kufanya mapitio ya Kanuni, na hatimaye kuzirekebisha na ndiyo kazi ambayo tunaifanya hivi sasa.

Mhe. Spika, Kamati yangu imekaa na kuyapitia mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni hizi na kimsingi tumekubaliana na mapendekezo hayo na kuyaunga mkono.

Pamoja na kuzingatiwa maoni yetu katika mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni hizo. Kamati imepitia, imejadili sana pamoja na wadau mbali mbali na baadhi ya mapendekezo yetu tumeyatoa wakati wa kupitia na tunamshukuru Mhe. Waziri kwa kuyakubali na kuyaweka kwenye mapendekezo haya ya Kanuni.

Mhe. Spika, Kamati yangu inapongeza kwa kukubali pendekezo letu la kuongeza wigo wa uwakilishi wa wanawake katika Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza ambao hivi sasa umekuwa katika kiwango cha chini. Hatua hii ni kubwa katika kuwashirikisha wanawake katika vyombo vya juu vya maamuzi, na kufanya hivyo sio kwa sababu ya kuwapendelea bali ni kutokana na wanawake kuwa na uwezo na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu na katika vyombo vyetu vya maamuzi.

Mhe. Spika, Kamati yangu pia imefurahishwa kuwekwa kwa uwazi suala kuanzishwa Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo ya Baraza la Wawakilishi. Kamati hii ambayo kwa hivi sasa imeanzishwa chini ya Kanuni ya 106 (L) imekuwa ipo kimaandishi na haijawekewa kazi zake maalum wala haina Wajumbe wa kufanya kazi hizo.

Kamati yangu inashauri katika mapendekezo haya ya kurekebisha Kanuni ni muhimu kuwekwa kazi za Kamati hiyo pamoja na muundo wake na kipindi ambacho kitakutana kufanya kazi zake.

Mhe. Spika, katika marekebisho haya ya Kanuni Kamati ya Sheria ndogo ndogo hivi sasa itajulikana kuwa ni Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo. Hivyo basi, Kamati yangu inakubaliana na pendekezo kuwa Kamati hii itakapoundwa iwe ndiyo Kamati dhamana ya kupitia, kupendekeza na hatimaye kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za kudumu za Baraza badala ya marekebisho hayo kuwasilishwa na Serikali kama inavyofanyika hivi sasa.

Mhe. Spika, katika Kanuni inayohusu utaratibu wa kuuliza maswali Barazani, Kamati yangu inapongeza kwa kufanywa marekebisho madogo ya Kanuni ya 39 kwa kuchunga nidhamu ya Wajumbe ya kuuliza maswali kwa niaba ya Wajumbe ambao hawapo.

Hata hivyo Kamati yangu inashauri kuwa endapo Mjumbe ataamua kuliondoa swali lake, na kwa kuwa Mjumbe huyo atakuwa ameshapewa taarifa ya lini swali hilo litajibiwa, basi kabla ya swali hilo kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli aliondoe kwa kutoa taarifa kwa Waziri husika, Katibu na Spika, ili kutoa nafasi kwa maswali mengine kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli.

Mhe. Spika, kimsingi marekebisho haya ni mengi, na Wajumbe wako wamepatiwa nakala, wamepitia na Kamati yangu imepitia, tumeridhika na kukubaliana nayo pamoja na ushauri wetu katika maeneo machache.

Hivyo nichukue tena fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambao tumeshirikiana katika kupitia mapendekezo haya, na naomba kwa umuhimu wa kazi hii waliyofanya niwataje kama ifuatavyo.

| | |
|---|---|
| Mhe. Ussi Jecha Simai | Mwenyekiti |
| Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Makamo Mwenyekiti |
| Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Mjumbe |
| Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Mjumbe |
| Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Mjumbe |
| Ndg Aziza Waziri Kheir | Katibu; na |
| Ndg Khamis Hamad Haji | Katibu |

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kukupongeza tena kwa umakini wako wa kuiwezesha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kupitia marekebisho haya ya Kanuni tukiwa pamoja na wadau na wataalamu, ambao wamewezesha Kamati kuelewa na kuwasilisha hotuba hii tukiwa tumeridhika.

Nawaomba Wajumbe wako waipitie na watafakari na hatimaye wapitishe Azimio hili ili Kanuni zetu hizi zikae vizuri zaidi katika kuendesha shughuli za Baraza.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo kwa niaba ya Mwenyekiti wetu wa Kamati Mhe. Ussi Jecha Simai ambaye anaendelea kupata nafuu juu ya mtihani wa maradhi, na tunamuombea Mwenyezi Mungu amjaalie yeye na wagonjwa wote afya njema na uzima. Nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Wanu Hafidh Ameir kwa kutoa maoni ya Kamati na kuunga mkono hoja juu ya Azimio hili. Waheshimiwa Wajumbe nimepata mchangiaji mmoja hadi sasa ambaye ni Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, lengo ilikuwa sio kuchangia, isipokuwa naomba kutumia Kanuni ya 64 kuomba Baraza lako Tukufu, kwamba

maazimio haya baada ya kwisha kuwasilishwa tupate muda basi wa kuweza kwenda kutafakari, na *In shaa Allah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atakapotujaalia tukaweza kurejea tena, ili Baraza linalokuja liweze kuja kukaa, kuangalia pamoja na kupitisha maazimio haya kwa mujibu wa mapendekezo ambayo yametolewa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba maelezo hayo na maazimio hayo tuyaweke mpaka Baraza la Wawakilishi linalofuata. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe sasa kumekuwa na hoja mbili. Hoja moja ya Azimio ambalo limeungwa mkono kwamba tujadili; na hoja ya pili kwamba tusijadili ila tuakhirishe. Sasa katika hali hiyo tunafanyaje?

Kanuni ni mali yetu Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo sisi ndio tunaoweza kusema kwamba basi tuache mpaka hapo baadaye, na sisi ndio tunaoweza kusema kwamba hapana, turekebishe.

Ni mali yetu, ila tu tukiacha kurekebisha maana yake Kanuni hii inaendelea, na haya yote ambayo tumeyapendekeza humu na wengine mkayaunga mkono kwamba basi tuyarekebishe, na Kamati ya Kanuni nayo ikasema hivyo hivyo wanaounga mkono hiyo hoja ya Azimio kwamba irekebishwe kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Nchi, sasa basi tuamue, ni mali yetu hii.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, sisi hatuna tatizo na hilo, isipokuwa tunaloliomba sio kwamba tunakataa hoja, hoja tunaikubali lakini tunaomba ule mjadala wake ukae katika kikao kinachokuja ili wale watakaokuja ndio wafaidi zaidi pamoja na *comments* zetu ambazo tumezitoa na wao waweze kutoa zao ili tutengeneze katika kikao cha mwanzo kitu kizuri zaidi kitakachokuwa kina manufaa, na kuweza kutumika kwa maslahi yetu sote. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Hatujaendelea na kufanya maamuzi, ilikusudiwa marekebisho haya yafanyike kwenye Baraza hili tulilonalo, kwa sababu sisi ndio ambao tumecheza na Kanuni hii kwa muda wote wa miaka mitano, tukajua matatizo ya hapa na pale, kwa hivyo ni sisi ndio tunaoelewa. Tukitaka tuwaachie Baraza lijalo *In shaa Allah* sisi sote humu ndani turudi! (*Makofi*)

Lakini maamuzi hayo bila ya shaka ni mwenyewe Mwenyezi Mungu na wananchi, inawezekana baadhi yetu tusirudi, *In shaa Allah* isitokee hivyo, wengine wanaweza wakarudi, wengine wasirudi.

Linakuja Baraza jipya, Baraza jipya katika hatua ya kwanza hasa Mkutano wa Kwanza kwa kawaida shughuli yake ni kuchagua Spika, Naibu Spika na viongozi wengine, kama tutaona ni muafaka kwa kipindi kile, kuapishana na baadaye kumuomba Mhe. Rais aje tena aje azindue Baraza kwa kawaida hiyo ndiyo kazi kubwa ya Mkutano wa Kwanza.

Kama tungekuwa tuna uhakika tunaorudi ni sisi sote tuliokuwemo humu ndani tungeweza tukaongeza kazi ili jambo hili tutakuwa tumepata muda wa kutosha, ambao sina hakika kama muda huo tutautumia kutafakari jambo hili au kutafakari namna ya kuweza kurudi humu ndani. Maana utaratibu wa kurudi humu ndani nao una mambo yake. Kwa maana hiyo tukiacha kujadili na kuamua leo maana yake Kanuni tunayokwenda nayo ni hii.

Pili kwenye Mkutano wa kwanza si aghalabu kuweza kuifanya kazi hii, wengine wanaweza wakawa ni wapya na tukaja tukawafikisha pahala tunawapa kazi ya uamuzi juu ya mambo ambayo kwao wao ni mapya kabisa, ndio tukaona kwamba ingekuwa ni vyema Baraza hili ambalo lina uelewa wa muda mkubwa basi tufanye maamuzi. Hiyo ndiyo namna ilivyokuwa, lakini vyenginevyo ingewezekana kabisa kufanya wakati mwengine wowote kama inavyoruhusu ile Kanuni tuliyoisoma hapa ya 157. Kwa hiyo ni kuamua kwamba tuendelee na hoja hii ili tupate Kanuni mpya kwa ajili ya Baraza jipya, ili wakati huo katika zile Semina zetu za awali itabidi tuwaeleze Wajumbe. Kanuni hii haitowaeleza Wajumbe Kanuni ambayo haijakuwepo bado. Tunaweza tukafanya Semina ili hatimaye waje waamue kama marekebisho haya yapo sawa.

Tuzingatie jambo hilo tu, lakini kimsingi sisi ndio wenye mali ya Kanuni, na sisi ndio tunaweza kuamua kwamba ni muafaka kurekebisha hivi sasa au si muafaka kurekebisha sasa, na tuje kurekebisha baadaye wakati wa Baraza jipya. Nataka tuyatafakari hayo ili tuweze kufanya maamuzi yaliyo sahihi.

Basi baada ya hayo niwaulize wale ambao wanataka tufanye marekebisho wakati huu wa Baraza hili la Nane na ni siku ya leo wanyanyue mikono. Hebu tuhesabu. Wale ambao wanaona tuakhirishe shughuli hii mpaka Baraza jipya la Tisa litakalokuja baadaye wanyanyue mikono. Haya Katibu nipe hesabu.

Matokeo ni kama ifuatavyo; wale ambao wanahitaji kwamba Baraza hili liendelee kujadili marekebisho haya idadi yao ni 13. Wale ambao wanaona tungeakhirisha shughuli hii mpaka Baraza lijalo ni 19. Kwa hiyo waliokubali kwamba shughuli hii ifanyike katika Baraza lijalo wameshinda! (*Makofi*)
Kwa hivyo tukubaliane kwamba shughuli hii inaakhirika mpaka Baraza lijalo. Waheshimiwa Wajumbe Mwenyezi Mungu akitujaalia kesho tunategemea tuwe na kikao kama kawaida Saa 3:00 tutakuwa na shughuli kidogo ambayo Mhe. Makamo

wa Pili wa Rais atakuja kuwasilisha hapa, lakini baadaye mnamo saa 9:30 wakati wa laasiri tumkaribishe Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili aje alihutubie Baraza hili, na hotuba yake itakuwa inaashiria kumalizika kwa uhai wa Baraza hili ambapo baada ya hapo atatoa tamko la kulivunja Baraza.

Kama tunavyoelewa Waheshimiwa Wajumbe tupo sisi tuliomo, haitakuwa na sura njema kuona kesho tutakuwa na Wajumbe kidogo. Kwa hivyo nawasihi na kuwaomba sana kuanzia kikao cha asubuhi cha saa 3:00, na pia Kikao cha pale laasiri saa 9:30, sisi tuliokubali kuendelea na kazi tuwe wengi wa kutosha humu ndani. Itakuwa ni aibu mbele ya wananchi, ni aibu mbele ya kiongozi wetu, kuja kuona kuna kiti chochote kitupu. Kwa hivyo nawaomba sana Waheshiniwa Wajumbe tuje kwa wakati. Haitopendeza hata kidogo Rais yupo hapa juu anaanza kuhutubia na wengine ndio kwanza wanajipenyeza, haitopendeza. Sote iwe tumo ndani humu kabla ya muda wa saa 9:30. Ratiba inaonesha kwamba sisi Wajumbe tunatakiwa tuwe tumeshakaa humu ndani saa 8:30 mchana. (*Makofi*)

Baada ya hapo mgeni wetu mmoja maalum tuliyoridhia aingie humu na ndani ataingia, baadaye Mhe. Rais na yeye pia ataingia ikifika saa 9:30 na kutakuwa na wageni wetu wengine wengi tuliowaalika ili Mhe. Rais afanye kazi yake kwa mujibu wa Katiba. Hilo ndilo ombi langu na naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tukubali hilo bila ya kukosa, ili kujiwekea hadhi mbele ya wananchi wetu lakini pia kutoa nidhamu na heshima kubwa kwa Mhe. Rais atakapokuja kulihutubia Baraza, lakini hata kabla ya pale ambapo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atatoa maelezo juu ya kazi yetu tuliyoifanya na muhtasari wa kazi tuliyoifanya kwa kipindi cha miaka mitano.

Waheshimiwa Wajumbe hayo ndiyo niliyokuwa nataka niwambie, lakini kuna jambo moja dogo muhimu ambalo litafanyika humu humu ndani nalo ilikuwa ni sehemu ya kazi yetu, ambalo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais anataka kutoa maelezo kwenu katika mfumo wa *briefing,* sio mfumo wa Baraza, lakini ili kuokoa muda mara baada ya kutoka humu ndani mimi Spika, Wajumbe wengine wote mtabaki humu ndani ili tumsikilize Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ana maelezo anayotaka kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe.

Baada ya hapo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa tusitishe shughuli zetu hadi kesho tarehe 26/06/2015 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 6:46 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/06/2015 saa 3:00 za asubuhi)*